# BreastScreen WA

Swahili Kiswahili

## Taarifa ya Uchunguzi wa Matiti – Inapatikana katika lugha zingine



### Kansa ya matiti - ukweli

Kansa ya matiti ni aina ya kansa inayotishia maisha kwa wanawake nchini Australia na haiwezi kuzuiwa.

**Sababu kubwa ya hatari inayopelekea kuwa na kansa ya matiti ni kuwa mwanamke na jinsi unapoendelea kuwa mzee.**

Kansa ya matiti ni kundi la seli zisizo za kawaida ambazo zinaendelea kukua na kuongezeka. Hatimaye seli hizi zinaweza kutengeneza uvimbe kwenye titi. Kama kansa haijaondolewa au kudhibitiwa basi seli za kansa zinaweza kuenea katika sehemu nyingine za mwili na zinaweza kusababisha kifo. Kugundua kansa ya matiti katika hatua ya mapema inaboresha nafasi ya matibabu yenye mafanikio.

### Ni nani anaweza kuwa na uchunguzi kupitia mammogram?


BreastScreen WA inatoa **BURE** uchunguzi wa mammogram kwa wanawake wenye miaka 40 au zaidi na wasiokuwa na dalili za magojwa. BreastScreen WA inawahimiza wanawake wenye umri wa **miaka 50 hadi 74** kuwa na uchunguzi wa **BURE** wa mammogram **kila baada ya miaka miwili.**

**Zaidi ya 75% ya kansa ya matiti hupatikana kwa wanawake wenye umri wa miaka 50 na zaidi.**

BreastScreen WA inaheshimu usiri wa kila mwanamke na heshima. Ni chaguo lako kuwa na uchunguzi wa x-ray ya matiti. Katika kufanya uamuzi huu unaweza kutaka kujadili hali yako na daktari wako.

### Nini maana ya uchunguzi wa mammogram?

Uchunguzi wa mammogram ni X-ray, au picha, ya ndani ya titi ya mwanamke. Uchunguzi wa mammogram huchunguza njia bora ya kuchunguza kansa ya matiti mapema.




Uchunguzi wa mammogram kugundua kansa ya matiti kabla wewe au daktari wako anaweza kuhisi.

### Uchunguzi wa mammogram unafanyika namna gani?

Matiti huwekwa kwa makini kwenye mashine ya X-ray na kufyinywa kwa sekunde chache wakati X-ray inachukuliwa. X-rays mbili huchukuliwa kwa kila titi, moja kutoka juu na moja kutoka upande.

Mfinyazo wa matiti ni muhimu ili picha iliyo wazi inaweza kuchukuliwa na kiasi kidogo cha mionzi hutumiwa (tazama picha hapa chini).

Mfinyazo waweza kufanya kutojisikia vizuri lakini huchukua sekunde chache tu. Unaweza kuuliza mpiga picha kuacha wakati wowote.




### Inakuwaje ninapotembelea BreastScreen WA kwa ajiri ya uchunguzi wa BURE wa mammogram?

Wafanyakazi wote wa kliniki za BreastScreen WA ni wanawake.

Wakati unafanyiwa mammogram, vaa nguo za vipande viwili, kama vile sketi au suruali na shati.

Usitumie poda ya Talcum au diodorani siku hiyo ya miadi yako.

Wakati utakapofika kwenye BreastScreen WA:

- Utakaribishwa na kuulizwa kujaza aina fulani ya fomu.
- Utaonyeshwa kwenye chumba cha mabadiliko na kuuliza kuondoa sidiria yako na kuweka nyuma yako juu; utapewa kanzu ziada inayotolewa kama unahitaji moja.
- Mpiga picha mwanamke atakuchukua wewe katika chumba cha X-ray na kuuliza baadhi ya maswali. Kisha baadaye atakuchukua X-rays mbili kwa kila titi.
- Mpiga picha atakuambia wakati wa kuondoka
- X-rays yako itapitiwa upya na angalau watu wawili ambao ni madaktari waliofuzu na kila juhudi itafnyika ili kuhakikisha wewe unapokea matokeo yako katika wiki mbili hadi tatu.
- Wakati mwingine wanawake wanaitwa kurudia X-rays nyingine. Ikiwa hii ni inatakiwa kwako BreastScreen WA watakuita ili kujadili hili na wewe.

**Ili kupata miadi piga 13 20 50**

## Ni wapi naweza kufanya uchunguzi wa mammogram?

BreastScreen WA ina huduma ya upimaji ya mjini, vijijini na huduma ya kuzunguka.

Ili kujua kituo cha karibu yako tembelea:

www.breastscreen.health.wa.gov.au/Breast-screening/ Breast-screening-locations

- Huduma nne za kuhamishika hufanyika vijijini kila baada ya miaka miwili. Kupata makadirio ya tarehe za kuzunguka tembelea: www.breastscreen.health.wa.gov.au/Breast-screening/Rural-and-remote-women
- Miadi ya jioni na Jumamosi inapatikana kwenye Kliniki nyingi.
- ♿ Ufikiaji wa kiti cha walemavu inapatikana kwenye BreastScreen WA.
- Wakalimani wa bure wanapatikana.

## Namna gani naweza kuomba miadi?

Ikiwa unahitaji msaada wa mkalimani, tafadhali pigia huduma ya Utafsiri na Ukalimani wa Lugha (TIS) kwanza kwa **13 14 50** na kuomba kuunganishwa na huduma ya kati ya BreastScreen WA kwa **13 20 50**.

Au piga simu **13 20 50** kwa ajiri ya miadi ya uchunguzi wa mammogram wa BURE (kwa gharama ya kupiga ya kawaida)

**Kufanya miadi kupitia mtandao kunapatikana** kwa miadi ya kawaida yote ya Kliniki za BreastScreen WA

**www.breastscreen.health.wa.gov.au**

## Miadi ya makundi

Miadi ya vikundi inapatikana kwa wanawake ambao wangependa kuhudhuria kama kikundi. Kwa maswali zaidi kuhusu kundi la uhifadhi Tafadhali simu **13 20 50.**

## Rasilimali zilizopo katika lugha zingine

BreastScreen WA ina rasilimali katika lugha zingine. Kuweza kuona zilizopo tembelea: www.breastscreen.health.wa.gov.au/Breast-screening/Multicultural-women

## Naweza kufanya nini pia?

Hata kama huwa unafanya mammogram ya mara kwa mara BreastScreen WA inahimiza wanawake wote kuweza kujua matiti yao.

Kufahamu hali ya matiti kunamaanisha kuweza kujua jinsi matiti yako yalivyo na kujisikia katika nyakati tofauti. Mabadiliko mengi kwenye matiti ni ya kawaida na yanatokana na mabadiliko ya homoni na jinsi unavyozidi kuzeeka. Ni muhimu kupata kujua mtazamo wa kawaida na kuhisi matiti yako, hivyo unaweza kutambua mabadiliko yoyote mapya au ya kawaida. Angalia katika kioo kwenye matiti yako na tazama matiti yako mara kwa mara.

Mabadiliko ya kuangalia yanajumuisha:

- Uvimbe mpya, uvimbe uliopo au kukonda kwa titi au eneo laubavu;
- Mabadiliko yoyote kwa chuchu ikiwa ni pamoja na, mchozo, kuchomeza, vidonda au kuwasha;
- Mabadiliko yoyote kwa ukubwa, sura au rangi ya chuchu au titi;
- Mabadiliko yoyote ya ngozi kama vile chunusi, uwekundu au upele; au
- Maumivu yoyote mapya, ya kawaida au ya kuendelea.

**Kama utagundua mabadiliko yoyote kati ya hayo haya kwenye matiti yako, vizuri uonane na daktari wako.**





Ni muhimu kuangalia tishu zote za matiti kutoka mfupa wa juu hadi chini ya mstari wa sidiria na eneo la chini ya mkono.


Government of Western Australia
North Metropolitan Health Service

BreastScreen WA
WA's only accredited screening service

BreastScreen AUSTRALIA
A joint Australian, State and Territory Government Program

HP000373 OCTOBER 2019

**BreastScreen WA**
Simu (08) 9323 6700 Faksi (08) 9323 6799 Barua pepe breastscreenwa@health.wa.gov.au
**Kufanya miadi 13 20 50**
Huduma ya taifa ya viziwi www.relayservice.gov.au Huduma ya Ukalimani na Utafisiri (TIS) 13 14 50